

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA**



MKUTANO WA KWANZA

YATOKANAYO NA KIKAO CHA TATU

19 NOVEMBA, 2015

MKUTANO WA KWANZA

YATOKANAYO NA KIKAO CHA TATU - TAREHE 19 NOVEMBA, 2015

I. DUA:

Saa 3.00 asubuhi Mheshimiwa Job Y. Ndugai (Spika) alisoma Dua na kuongoza Kikao cha Bunge.

II. KUTHIBITISHA UTEUZI WA WAZIRI MKUU:

Mhe. Spika aliwataarifu Waheshimiwa Wabunge kuwa mpaka wakati huo hajapokea Barua ya Mheshimiwa Rais yenye jina la Mbunge anayependekezwa kuwa Waziri Mkuu.

Saa 3.35 Asubuhi Mpambe wa Rais aliingia ndani ya ukumbi wa Bunge na kumpatia Mheshimiwa Spika bahasha yenye barua kutoka kwa Mheshimiwaa Rais.

Mheshimiwa Spika aliifungua barua na kuliarifu Bunge kuwa Mheshimiwa Rais amemteua Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

III. KUSITISHA SHUGHULI ZA BUNGE:

Kwa kuwa kanuni ya 25 inaelekeza kwamba baada ya Mheshimiwa Spika kutaja jina la Mbunge anayependekezwa kuwa Waziri Mkuu, Mwanasheria Mkuu wa Serikali atatoa Hoja kuliomba Bunge lithibitishe uteuzi huo na kwa kuwa hata Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu hakuwa anafahamu jina la Mbunge anayependekezwa hivyo hajaandaa maelezo ya Hoja yake ikiwa ni pamoja na wasifu wa Mbunge husika hivyo Mheshimiwa Spika aliamua kusitisha shughuli za Bunge kwa dakika 45 ili kumpa nafasi Mwanasherria Mkuu wa Serikali akaandae maelezo ya Hoja yake.

IV. BUNGE KUREJEA:

Shughuli za Bunge ziliendela saa 3:05 Asubuhi ambapo Mwansheria Mkuu wa Serikali kutoa hoja ya kuliomba Bunge lithibitishe uteuzi wa Waziri Mkuu. Wabunge wafuatao walichangia hoja hiyo:-

1. Mhe. William Vangimembe Lukuvi, Mb
2. Mhe. Jenista Joakim Mhagama, Mb
3. Mhe. Dkt. Hamis Andrea Kigwangala, Mb
4. Mhe. Alphaxard Kangi Lugola, Mb
5. Mhe. Adrew John Chenge, Mb

Baada ya wachangiaji kukamilika Katibu wa Bunge alitoa maelezo ya utaratibu wa kuthibitisha uteuzi wa Waziri Mkuu. Kabla ya zoezi la kuthibitisha Uteuzi wa Waziri Mkuu Katibu wa Bunge alitaja idadi ya Wabunge kikatiba kuwa ni 394 na walioapishwa mpaka siku hiyo ni Wabunge 369 na kwamba akidi ni Wabunge 184 ambapo waliopo ndani ya ukumbi ni 351 hivyo akidi kwa zoezi la upigaj kura imetimia. Baada ya maelekezo hayo kura zilipigwa.

V. UCHAGUZI WA NAIBU SPIKA:

Wakati zoezi la kuhesabu kura za kuthibitisha uteuzi wa Waziri Mkuu linaendelea Spika alielekeza Shughuli ya uchaguzi wa Naibu Spika iendelee.

Katibu wa Bunge alitoa maelezo ya taratibu za uchaguzi wa Naibu Spika na kuwataja wagombea wa nafasi hiyo kuwa ni Mheshimiwa Magdalena Hamisi Sakaya (CUF) na Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson.

Wagombea waliitwa mmoja baada ya mwингine ili kujieleza na kuulizwa maswali, kisha zoezi la kupiga kura lilifanyika.

VI. MATOKEO YA KURA ZA KUTHITISHA UTEUZI WA WAZIRI MKUU:

Idadi ya kura zilizopigwa	357
Kura zilizoharibika	2 sawa na 0.06%
Kura za NDIYO	258 sawa na 73.5%

Mhe. Spika aliwatangazia Wabunge kuwa Bunge limethibitisha Uteuzi wa Mhe. Kassimu Majaliwa Majaliwa (Mb) kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Waziri Mkuu Mtule alipewa fursa ya kutoa neno la shukrani.

VII. MATOKEO YA UCHAGUZI WA NAIBU SPIKA:

Idadi ya kura zilizpingwa	351
Kura zilizoharibika	0
Kura halali	351

Mhe. Magdalena Hamisi Sakaya – 101 sawa na 28.8 %

Mhe. Dkt. Tulia A. Mwansasu – 250 sawa na asilimia 71.2%

Mhe. Spika alimtangaza Mhe. Dkt. Tulia Ackson kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Dkt. Tulia Ackson alipewa fursa ya kutoa neno la shukrani.

VIII. KIAPO CHA NAIBU SPIKA:

Mhe. Dkt. Tulia Ackson aliapa kiapo cha kuwa Naibu Spika.

IX. KUAHIRISHA SHUGHULI ZA BUNGE:

Saa 7:25 mchana Shughuli za Bunge ziliahirishwa hadi Ijumaa tarehe 20 Novemba, 2015 saa 9:00 alasiri.

**DODOMA
19 NOVEMBA, 2015**

**DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE**